# CLASS 8 END TERM 3 DECEMBER 2021

## KISWAHILI

***Jaza nafasi 1-15 ukitumia neno sahihi kati ya yale uliyopewa.***

____1____, huduma milele. Haidumu tu vitabuni, ____2____ hata pia akilini kwa wale waliosoma na si kusoma mara moja tu bali ____3____. Tabia ya kusomasoma inafaa kukuzwa na kutunzwa kama vile mimea itunzwavyo kwa ____4____ na mbolea. Elimu ni kitu muhimu kwa mwanadamu. Elimu ____5____ katika shule au vyuo au taasisi za elimu tu bali ni jambo linaloanza mtu anapozaliwa na kukoma tu____6____.

Katika juhudi za serikali za kupambana na kutojua kusoma na kuandika miongoni mwa hatua au mbinu ____7____ ni pamoja na utoaji wa elimu ya bure na kutoa huduma za maktaba kote nchini kwa lengo la kuwafikia hata wale wanaoishi mashambani ili ____8____ viwango vya elimu.

1. **A.** Cha kuzama hakina rubani **B.** Alisifuye jua limemwangazia **C.** Ushikwapo shikamana **D.** Liandikwalo halifutiki
2. **A.** bali **B.** hata **C.** ila **D.** ikawa
3. **A.** mbio mbio **B.** tena na tena **C.** abadan kataani **D.** katu
4. **A.** kupigwa dawa **B.** kutiwa matuta **C.** kutiwa maji **D.** kutiwa udonge
5. **A.** hupatikana **B.** husomewa **C.** huonekana **D.** haipatikani
6. **A.** akienda mrama **B.** akila mwata **C.** akikata kamba **D.** akikanyaga chechele
7. **A.** iliyopendezwa **B.** zilizopendekezwa **C.** zitakazopendekezwa **D.** iliyopendekezwa
8. **A.** kuimarisha **B.** kukamilisha **C.** kumaliza **D.** kupuuza

Wakati ulionekana kupita polepole usiku ____9____. Nilikuwa na bashasha kuu kuiona siku ____10____. Ilikuwa ni siku ambayo ilikuwa na umuhimu mkubwa maishani____11____. Siku hiyo, ningesafiri____12____ ndege kwa mara yangu ya kwanza kwenda ughaibuni kuyaendeleza masomo yangu. Jogoo ____13____ kwanza ____14____, mimi ____15____ niliyekuwa wa kwanza kulitupa mbali blanketi langu.

9. **A.** huo **B.** huyo **C.** hio **D.** hiyo
10. **A.** iliyotangulia **B.** iliyoisha **C.** inayokuja **D.** iliyofuatia
11. **A.** mwangu **B.** kwangu **C.** pangu **D.** zangu
12. **A.** na **B.** kwa **C.** pamoja na **D.** katikati
13. **A.** ya **B.** la **C.** wa **D.** za
14. **A.** alipowika **B.** alipororoma **C.** alipoita **D.** alipokoroma
15. **A.** ndiye **B.** ndie **C.** ndiyo **D.** ndimi

***Kutoka swali la 16-30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Ni sentensi gani isiyo sahihi kisarufi?
    A. Mchele uliyopikwa si mtamu.
    B. Changu huuzwa ghali siku hizi.
    C. Ukwenzi uliosheheni ulidhihirisha hofu na maumivu.
    D. Kifaru aliyetoroka mbugani alishikwa na kurejeshwa mara moja.
17. Ni matumizi yapi ya **ji** yanayojitokeza katika sentensi hii
    <u>**Ji**</u>sahani lili**ji**angusha likavunjika vigaevigae
    A. udogo, ukubwa B. ukubwa, nafsi
    C. hali, udogo D. mtendaji, nafsi
18. Teua sentensi yenye dhana ya masharti
    A. Tukutu amekuwa akiwababaisha wenzake darasani.
    B. Daktari amekuwa akiwashauri waathiriwa wa UKIMWI.
    C. Maria asipofika hapa mapema ataadhibiwa.
    D. Ungemwona angekudanganya umpe pesa.
19. Chagua matumizi ya **'ni'** ya kuonyesha nafsi
    A. Maria ni bingwa.
    B. Sokoni si mbali.
    C. Simameni mkamkaribishe mgeni.
    D. Angeniita ningeitika.
20. **Yakinisha sentensi hii**
    ***Tusipoondoka hatutafaulu kumpata***
    A. Hatungeondoka tungefaulu kumpata
    B. Tusingeondoka tusingefaulu kumpata
    C. Tukiondoka tutafaulu kumpata
    D. Tuliondoka tukampata.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

21. Chagua kundi lenye maradhi pekee
A. Kifaduro, malale, pumu, muhina.
B. Tetekuwanga,ukosandisha, malaria, tete.
C. Upele, ukoma, ukambi, ukiwa.
D. Kisukari, kifua kikuu, kiharusi, mwangwi.

22. **Andika usemi wa taarifa wa**
*"Safari yetu ni ya kesho," mjomba alisema*
A. Mjomba alisema kuwa safari yao ni ya siku iliyotangulia.
B. Mjomba alisema kuwa safari yao ni ya kesho.
C. Mjomba alisema kuwa safari yetu ni ya siku ifuatayo.
D. Mjomba alisema kuwa safari yao ilikuwa ya siku iliyofuata

23. Ni sentensi ipi ambayo imetumia **kwa** ya kuonyesha jumla?
A. Waliadhibiwa kwa utovu wa nidhamu.
B. Alichelewa kazini kwa kukosa gari la kusafiria.
C. Wazee kwa vijana huhimizwa kuheshimu sheria.
D. Alinyolewa kwa wembe akawa mfano wa kioo.

24. Chagua kundi lenye vivumishi pekee
A. labda, mpaka, na hivyo
B. zangu, mzuri, wote, watatu
C. taratibu, kijeshi, sana, vibaya
D. wote, wazuri, mnyonge, afanalek!

25. Bainisha maneno yaliyopigiwa mstari
*Mtu mwenye kichwa kidogo anafua chuma.*
A. Kivumishi, kivumishi, kitenzi
B. Kiashiria, kielezi, kitenzi
C. Kitenzi, kiwakilishi, kivumishi
D. Kisifa, kiarifa, kibadala

26. Nywele zinazozuia vumbi kuingia machoni ni
A. masharubu
B. kope
C. nyusi
D. mavazi

27. Ni tashbihi ipi inayoafikiana na maelezo haya?
*"Kutokeza na kuendelea vizuri kwa haraka" ni*
A. chipuka kama majani
B. chanua kama waridi
C. chanua kama mgomba
D. chipuka kama uyoga

28. Ni ipi ndiyo maana ya methali hii?
*Sikio la kufa halisiki dawa*
A. Asiyesikia haambiwi.
B. Sikio la kufa, halitibiwi.
C. Asiyetii ni vigumu kumkanya.
D. Asiyesikia hasikii.

29. Mwalimu alianguka chini ya gari
Maneno yaliyopigiwa mstari yametumikaje?
A. Kielezi cha mahali.
B. Kihusishi cha mahali.
C. Kielezi cha nomino.
D. Kiunganishi cha mahali.

30. Teua sentensi iliyo katika hali timilifu
A. Wageni watakapofika watapokelewa.
B. Hawajakuwa wakifanya kazi vizuri.
C. Maria huimba vizuri akiwa peke yake.
D. Naomba unionyeshe vyoo vya shule hii.

**Soma ufahamu ufuataao kisha ujibu maswali 31-40.**

"Mkuu wa afya jimboni, wageni wako na wazazi kwa jumla sabalkheri?Mpo?kwema? Ninachukua fursa hii adimu na adhimu kuwahutubia kuhusu watoto wetu na umuhimu wao. Mimi kama mtetezi wa watoto nchini nimekuwa nikikosa usingizi mara kwa mara ninapowawazia watoto wanavyoteseka huko nje.

Mtoto ni zawadi apewayo mtu na Mungu wake. Katika hali halisi, mtu anapotunukiwa, hukitunza chochote alichopewa kwa kila hali. Ikiwa ni kito cha dhahabu au almasi, hufungiwa kwa usiri mkubwa kwenye kasha, kisha huhifadhiwa pahali pazuri. Sisemi tuwafungie watoto wetu kwenye masanduku na kuwaficha. La hasha! Ninamaanisha kuwa, mtoto aheshimiwe na atendewe mambo yanayostahiki.

Ni jukumu la kila mzazi au mlezi wa mtoto kutambua kuwa mtoto ana haki ya kuishi. Kitendo cha kuua ni kinyume cha sheria kwa mujibu wa katiba yetu. Si haki kumnyima mtoto nafasi ya kuishi. Nyinyi mnajua kuna visa vingi vya wanawake ambao huavya mimba na kukatiza uhai wa watoto wangali matumboni mwao. Watu kama hao si tofauti na wauaji. Wengine huwaua watoto wao kwa kuwachoma au kuwakaba koo. Si ni kweli hata katika vitabu vitakatifu mauaji ya binadamu ni haramu.

Tujue hivi, mtoto anapaswa kuelimishwa. Maisha ya kisasa hayawezekani bila elimu. Ajira bora zenye mishahara mikubwa ni za wale walioelimika. Inasikitisha kuona wazazi, nyinyi mkichelea kumpeleka mtoto papetolewapo elimu. Aghalabu watoto huamriwa kwenda kufanya kazi kwenye mashamba ya mabwenyeye na wengine hasa wasichana, mara tu wakivunja ungo, huozwa.

Wazazi mnawapenda watoto wenu? Msisikie tu, jiulize ama kweli unampenda mwanao kikweli. Wengine hamjali hambali. Anasa za dunia zimewanasa na kuwateka kiasi cha kuwatenganisha na watoto wenu. Hela zinawafanya kuajili liamba na kurejea usiku wa giza la mashetani. Watoto wengine husumbuka kisaikolojia kiasi cha kuamua kujiangamiza kutokana na malezi duni. Wazazi, tuwapeni watoto wetu mapenzi yanayofaa ili nao watuamini na kututhamini siku za halafu. Husemwa, mwana wa yungi hulewa, seuze wa mlimwengu?

Mbali na hayo, watoto wanahitaji kulishwa na si kulishwa tu bali wapewe lishe bora bali si bora lishe. Wapewe chakula chenye virutubishi vinavyohitajika mwilini. Chakula bora humfanya mtoto awe buheri wa afya. Tukiwanyima chakula, wataenda kujitafutia. Watazurura vichochoroni na kule mitaani kama lofa au mbwakoko. Huko ndiko watakakokutania na walimwengu waliotumia mihadarati wakachakaramka. Aisee! Dunia ni tambara bovu.

Mtu asiye na kivazi mwilini ni chakaramu. Watoto wetu wanahitaji kuvishwa vizuri. Mwanafunzi aendapo shuleni ni ibada avalie sare. Iwapo watoto wanaenda mchezo kwa mfano kandanda, basi wawe na majezi na daluga. Siku za kuenda maabadini, wavalie mavazi bora ya siku hiyo. Ni wajibu wetu jamani.

Mwisho kabisa, jueni kuwa maneno ya watoto si ya kupuuza. Wakati mwingine ni vyema wapewe nafasi ya kujiamulia na kujieleza. Ni vyema kumsikiliza mtoto kwani huenda akawa na matatizo fulani aliyotoka apewe msaada. Ni matumaini yangu kuwa tukizipa haki za watoto kipaumbele tutauimarisha mustakabali wao. Asanteni kwa kunisikiliza. Mungu mwenye rehema awabariki mnapojiandaa kuwalea watoto wenu kwa njia zifaazo.

**31.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza, ni sahihi kusema
A. waliohudhuria mkutano walikuwa wageni wa kitaifa pekee.
B. wote waliokuwa kwenye mkutano walikuwa watetezi wa haki za watoto.
C. mhutubu hajawahi kulala kwa kuwa watoto huko nje wamekuwa wakiteswa.
D. hatibu amekuwa akwazia namna watoto wanavyoteseka kote.

**32.** Ni kwa nini mtu hukitunza kitu alichopewa kama zawadi?
A. Kwa sababu anakithamini sana
B. Kwa kuwa ilikuwa tu ni zawadi
C. Maadamu anakichukia sana
D. Kwa vile kitu hicho ni sharti akirudishe baadaye

**33.** Neno <u>kito</u> limepigiwa mstari. Ipi ndiyo maana yake?
A. Dhahabu
B. Almasi
C. Jiwe la thamani
D. Zawadi apewayo mtu

**34.** Kulingana na ufahamu;
A. ili tuwatunze watoto wetu vizuri, sharti tuwafungie.
B. hakuna kitu chochote muhimu isipokuwa dhahabu na almasi.
C. mtoto anastahili kutunzwa na kuthaminiwa kama kito.
D. makasha ndiyo hutumiwa kuhifadhia vitu vya thamani.

**35.** Kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu;
A. wanaume hawaruhusiwi kuwatoa wengine uhai.
B. hakuna mtu yeyote aliye na haki kisheria kuangamiza mtu yeyote.
C. wanawake hawana haki ya kuwatoa wanawe uhai.
D. ikilazimu unaweza kumwua mtu endapo unayatetea maisha yako.

**36.** Ni nahau gani isiyomaanisha kufariki?
A. Enda na ulele ngoma.
B. Kata kamba.
C. Fuata njia ya marahaba.
D. Enda pepe.

**37.** Ni haki ipi nyingine ya mtoto ambayo haijatajwa kwenye ufahamu?
A. Haki ya kuelimishwa
B. Haki ya kivishwa
C. Haki ya kupendwa
D. Haki ya kulishwa

**38.** Watu hutekeleza mauaji kwa njia hizi kwa mujibu wa taarifa isipokuwa
A. kuwapa sumu
B. kuavya mimba
C. kuwachoma watoto
D. kuwakaba koo

**39.** Watoto watakapokwenda kujitafutia chakula
A. watachoka sana
B. huenda wakatekwa nyara
C. watajipata wakitangamana na watumizi wa mihadarati
D. watatoroka na kutoweza kurudi nyumbani

**40.** Ni vyema kumsikiliza mtoto anapotuzungumzia kwani
A. huwa amedhulumiwa.
B. huenda ana jambo linalohitaji kushughulikiwa
C. mara nyingi huwa amechokozwa
D. husumbua na hahitaji kusikilizwa

***<u>Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41-50.</u>***

Mali nyingi na pesa nyingi ni nzuri lakini pesa au mali nyingi pekee haziwezi zikatosheleza mahitaji yote ya mtu. Mungu hamnyimi mja yote. Wengine ni matajiri wa mali lakini maskini wa utu ilhali wengine ni matajiri wa utu na hekima ingawa ni maskini wa mali. Hivyo basi ni vyema kumweshimu binadamu yeyote yule ingawa amepungukiwa kwa namna fulani. Husemwa, aliyekupa kiti ndiye aliyenipa kumbi.

Bwana Bosi, licha ya kuwa na mashangingi ya magari, alitawalwa na Iblis kiasi cha kutowabeba wanakijiji walipohitaji msaada wa kubebwa. Wanakijiji maskini hohehahe wangekanyaga wapi mwanzo wakiwa wamekanyaga chini? Wangelichafua gari lake Bwana Bosi eti!S hata wengine walikuwa wamevamiwa na tekenya? Na watoto wake ambao sasa wanaanza kuinukia na kufunzwa kuendesha magari pia walimwiga baba yao. Haidhuru, mtoto wa nyoka ni nyoka.

Mtashi hana kinyongo na hajapowaswa hakomi. Wahitaji wale walijikuta kwake kila uchao kutafuta vibarua au <u>makombo</u>. Vilevile magari yale ya Bwana Bosi yalipokwama msimu wa masika, walijikuta wakimsaidia kuyasukuma ili kuhakikisha kuwa Bwana huyo ameendelea na safari. Haya ya kumpa mkono Bwana Bosi yaliendelea kwa muda mrefu bila ya yeye kubadili mtazamo wake. Kwake, wanyonge wale



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

walimsaidia kwa sababu walimhitaji yeye. "kunifanyia kazi si wanataka unga?"

Mmoja wa wanakijiji siku moja aliibuka na wazo kuwa wakati wa mvua gari lake lisikwamuliwe. Kama kawaida yake aliendesha gari lake na lilipokwama naye akakwama ndani. Si kuna watu wa kumkwamulia gari! Alikaa ndani, kama ilivyo desturi yake. Vioo akavipandisha akawasubiri wapita njia wale. Hakuamini macho yake alipowaona watu wale wakimpita. Ikambidi ashuke garini na kuvikanyagisha viatu vyake vya bei chini. Hili liliendelea msimu mzima. Ilimbidi awe akisubiri mvua ikese ndipo gari likwamke. Juhudi za wanawe wawili za kulikwamua hazikuzaa matunda yoyote. Baadhi ya vibarua walijaribu kuzisusia kazi shambani mwake lakini uhitaji uliwarejesha palepale shambani. Hata baada ya hayo yote, Bwana Bosi hakuguswa mshipa.

Labda dawa ya uhasama si uhasama. Kituko kipya ndicho kilimfanya Bwana Bosi akubali kunywea. Siku moja akiwa mjini akiendelea kuokota malipo katika majumba yake, alisikia kuwa kuna majambazi waliokuwa wakisakwa na wanakijiji na walikuwa wamejificha katika pango moja karibu na kwake. Hilo halikumshtua kwani kwake palikuwa na walinzi waliohitimu na majibwa makali. Tena boma lake lilizungushiwa nyaya za umeme. Wanakijiji walijitahidi na kuwanasa watu wale. Umma wenye ghadhabu uliwaua wawili na kumpokeza mwengine kichapo cha mbwa kutabawali msikitini ila wakaamua kutomwua ili wamhoji.

Baada ya madhila ya muda, aliamua kujieleza dhahiri shahiri ili kuyaokoa maisha yake. Alieleza kuwa walikuwa wametumwa na mmoja wa washindani wa Bwana Bosi ili wamwue. Wangemvizia njiani. Ile ingekuwa siku yake ya mwisho kuishi kwa mujibu wa runinga aliyoitazama. Bwana Bosi aliona kifo kwa macho yake na wanakijiji ndio waliomwokoa. Wale aliowachukia kama kizazi kisicho na thamani yoyote, sasa walimwokoa. Hali hii ilimgusa pakubwa. Palepale alikimbilia kijijini na kuliegesha gari lake karibu na umati uliokuwa bado ukijadili yaliyojiri.

Aliingilia maongezi yale. Wanakijiji hawakujua waanzie wapi kwa kuwa hawakujua yeye huongea na maskini. Huku amejawa na simanzi aliwaomba waandamane naye hadi kwenye kituo cha polisi. Hakusahau kuwashukuru na kuwaomba msamaha kwa jinsi alivyowadharau awali. Hawakujua namna ya kumjibu ila kukubali kuandamana naye kuyaelezea yote. Keshoye, Bwana Bosi alikuwa akiwaomba watu waingie garini awafikishe walikokuwa wakienda. Alianza hata kuyatumia mengine kuwachukua vibarua wakielekea kwake shambani. Ujira nao aliuongeza <u>maradufu</u> na kuamuru hata wawe wakipewa chamcha na kufanya kazi saa chache. Kumbe Bwana Bosi aligundua kuwa naye alikuwa na umaskini wa aina yake.

---

**41.** Kwa nini Bwana Bosi hasa hakuwabeba wanakijiji katika magari yake?
A. Bwana Bosi aliwathamini sana wanakijiji.
B. Bwana Bosi aliwabeza wanakijiji.
C. Wanakijiji walimwogopa Bwana Bosi.
D. Magari yake yalikuwa ya kifahari.

**42.** Matatizo mawili ya kijiji hiki yaliyojitokeza
A. vimelea na ufukara
B. dharau na vimelea
C. umaskini na matope
D. barabara mbovu na utajiri

**43.** Neno <u>makombo</u> limetumiwa katika ufahamu. Lina maana kuwa
A. chakula kilicholala.
B. msaada wa pesa.
C. kazi za muda mfupi.
D. chakula kilichobaki.

**44.** Wanakijiji walimsukumia Bwana Bosi gari
A. ili awatafutie mali
B. kutokana na ubinadamu wao
C. kwa sababu walikuwa wakimwogopa Bwana Bosi
D. kwa sababu walimpenda sana Bwana Bosi

**45.** ...lilipokwama naye akakwama ndani."Kauli hii inaonyesha wazi kwamba Bwana Bosi...
A. hakutangamana na wanakijiji.
B. hakujali kuchelewa.
C. alikuwa tajiri sana.
D. hakutaka kukanyaga matope

**46.** Mvua kukesa kunyesha ni kufanya nini?
A. Kuacha kunyesha
B. Kunyesha mfululizo
C. Kunyesha kidogo kidogo
D. Kunyesha ikiacha

**47.** Bwana Bosi hakujishughulisha sana na taarifa za majambazi kwa kuwa
A. hakuwa na maadui wowote.
B. aliamini kuwa wanakijiji wangemlinda.
C. usalama ulidhibitiwa vizuri nyumbani kwake.
D. alijua hakuna yeyote ambaye angemdhuru.

**48.** "Wale aliowachukulia kuwa kizazi kisicho na thamani sasa walimwokoa" Ni methali gani inayoweza kuelezea kauli hii?
A. Mtu ni watu.
B. Baniani mbaya kiatu chake dawa.
C. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.
D. Bura yangu siibadili na rehani.

**49.** Ujira uliongezwa "maradufu" ni kumaanisha kuwa aliwaongeza
A. mara tatu zaidi
B. mara mbili zaidi
C. mara nne zaidi
D. mara moja zaidi

**50.** Bwana Bosi aligundua kuwa alikuwa na umaskini gani?
A. Ukarimu wake.
B. Kulikuwa na matajiri zaidi yake.
C. Hakuwa na utu.
D. Asingejitosheleza kwa hali yoyote.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com